TANGAZO LA SERIKALI NA. 754 la tarehe 30/8/2024

SHERIA YA MIPANGO MIJI,

(SURA YA 355)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 8(1) na 23(1))*

AMRI YA KURASIMISHA MAKAZI YASIYOPANGWA ENEO LA NKINDWABIYE NA SONGAMBELE YA MWAKA, 2024

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Kurasimisha Makazi Yasiyopangwa eneo la Nkindwabiye na Songambele ya mwaka, 2024.

Utangazaji wa Eneo la Upangaji Sura 355

2. Eneo lililoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa eneo la upangaji (Mpango wa Urasimishaji) kwa madhumuni ya Sheria ya Mipango Miji.

Mpango katika Eneo la kwenye Jedwali

3. Mipango kina katika eneo lililoainishwa kwenye Jedwali itaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipango Miji na Mkurugenzi wa walmashauri ya wilaya ya Bariadi.

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

Eneo la urasimishaji lipo ndani ya mipaka ifuatayo:-

“Unaanzia kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba NKB1 yenye majira – nukta 634594.8MS, 9722478.35KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Magharibi katika uelekeo wa KS227047’0”MG kwa umbali wa kilomita 0.65 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba NKB2 yenye majira – nukta 634112.85MS, 9721975.26KZ; baada ya

hapo mpaka unaelekea Kusini - Magharibi katika uelekeo wa KS152054’0”MG kwa umbali wa kilomita 0.42 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba NKB3 yenye majira – nukta 633715.47MS, 9721853.01KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Magharibi katika uelekeo wa KZ342031’50”MG kwa umbali wa kilomita 0.255 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba PIN2 yenye majira – nukta 633639MS, 9722096KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Magharibi katika uelekeo wa KZ31606’52”MG kwa umbali wa kilomita 0.78 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba NKB4 yenye majira – nukta 633100.35MS, 9722656.02KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Mashariki katika uelekeo wa KZ22016’49”MS kwa umbali wa kilomita 1.18 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba NKB5 yenye majira – nukta 634190.2MS, 9723096.8KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Mashariki katika uelekeo wa KS149036’54”MS kwa umbali wa kilomita 0.79 hadi ulipoanzia.”

Dodoma,
14 Agosti, 2024

DEOGRATIUS JOHN NDEJEMBI
*Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi*